**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

**ISO 9001:2015 Certified**

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

## UFAFANUZI KUHUSU TANGAZO LA VIAMBATO VYA VIPODOZI VILIVYOPIGWA MARUFUKU

**Dar es Salaam, 05 Mei, 2022**

Hivi karibuni Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilitoa tangazo kuhusu viambato vililivyopigwa marufuku kutumika katika vipodozi. Kufuatia tangazo hilo, wananchi na wadau wamekuwa wakiuliza maswali pamoja na kuomba na kupata ufafanuzi juu ya masuala mbalimbali kuhusu vipodozi.

Katika kutekeleza majukumu yake Shirika la Viwango Tanzania linazingatia Sheria ya Viwango Na.2 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Bunge kupitia Sheria ya Fedha Na. 8 ya mwaka 2019, Kanuni zilizoundwa chini ya Sheria ya Viwango pamoja na viwango vya kitaifa. Kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha Na.8 ya mwaka 2019, Shirika limepewa mamlaka ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi.

Katika kudhibiti ubora na usalama wa vipodozi, Shirika hutumia viwango vya bidhaa husika na miongoni mwa viwango hivyo ni kiwango cha lazima (*compulsory standard*) namba ***TZS 638:2014*** ambacho pamoja na mambo mengine kimeelekeza viambato vinavyoruhusiwa kutumika kwa kiasi maalumu na vile visivyoruhusiwa kabisa katika uzalishaji wa vipodozi. Kuzuiwa au kuruhusiwa kwa matumizi ya viambato hivyo hutokana na matokeo ya tafiti mbalimbali zinazofanyika.

Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa hivi karibuni juu ya viambato ambavyo vinaruhusiwa kutumika kwa masharti ya kiasi maalumu , imebainika kwamba matumizi ya muda mrefu ya baadhi ya viambato hivyo yanaweza kusababisha madhara ya kiafya kwa watumiaji na hivyo kufikia uamuzi wa kuzuia matumizi ya viambato hivyo katika utengenezaji wa vipodozi. Viambato vilivyozuiwa vinafahamika kwa majina ya ***Zinc pyrithione, Butyphenyl methypropional*** *na* ***Sodium hydroxymethylglycinate.***

**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma /
Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/
+255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF,
Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF,
Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na:
+255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2804023

Kufuatia zuio hilo la kitaalamu, Shirika la Viwango la Tanzania tulitoa taarifa kwa umma kudhibiti matumizi ya viambato tajwa ikiwemo uingizaji wa vipodozi vyenye viambato hivyo. Hata hivyo Shirika litaendelea kutoa elimu kwa wazalishaji, waagizaji na jamii kwa jumla ili kuleta uelewa wa pamoja na kuepusha madhara yanayoweza kujitokea kutokana na matumizi ya bidhaa zenye viambato hivyo.

Aidha, Shirika linatoa muda wa miezi mitatu kwa waagizaji, wasambazaji na wazalishaji wa vipodozi kufanya marekebisho ya kanuni za uzalishaji (*reformulation*) na kuijulisha TBS. Kwa waagizaji ambao bidhaa zao zilisajiliwa kabla ya katazo wanaelekezwa kusitisha uagizaji wa bidhaa zenye viambato hivyo kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **+0800110827.**

Imetolewa na:

Gladness H. Kaseka
**Meneja Uhusiano na Masoko**


**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma /
Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/
+255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na:
+255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na:
+255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na:
+255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na:
+255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2804023


Barua zote ziandikwe kwa **MKURUGENZI MKUU**